

JINA.....NAMBARI.....

SHULE.....SAHIHI.....

TAREHE.....

102/1

KISWAHILI

KARATASI YA 1

INSHA

MACHI/ APRILI 2015

MUDA: SAA 1  $\frac{3}{4}$

## **TATHMINI YA PAMOJA YA LAINAKU**

*Cheti cha Kuhitimu Elimu ya Sekondari (K.C.S.E)*

102/1

KISWAHILI

KARATASI YA 1

INSHA

MACHI/ APRILI 2015

MUDA: SAA 1  $\frac{3}{4}$

MAAGIZO

1. Andika insha mbili
2. Insha ya kwanza ni ya **lazima**
3. Kisha chagua insha moja nyingine kutoka kwa hizo tatu zilizobakia
4. Kila insha isipungue maneno 400.
5. Kila insha ina alama 20
6. Kila insha lazima iandikwe kwa kugha ya Kiswahili

### **KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE**

1	2	3	4	JUMLA

1. Unyakuzi wa ardhi umekuwa swala tata nchini katika siku za hivi majuzi. Andika tahariri ya gazeti la Mzalendo huku ukipendekeza suluhisho kwa tatizo hili.
2. Udanganyifu katika mitihani ya kitaifa umeleta madhara kwa wanafunzi. Eleza
3. Ng'ombe akivunjika mguu malishoni hujikokota zizini.
4. Tunga kisa kitakachomalizikia kwa:  
.....hapo ndipo nilipogundua kwamba Bahati alikuwa moto wa kuotea mbali.

JINA.....NAMBARI.....

SHULE.....SAHIHI.....

TAREHE.....

102/2

KISWAHILI

KARATASI YA 2

LUGHA

MACHI/ APRILI 2015

MUDA: SAA 2 ½

## **TATHMINI YA PAMOJA YA LAINAKU**

*Cheti cha Kuhitimu Elimu ya Sekondari (K.C.S.E)*

102/2

KISWAHILI

KARATASI YA 2

LUGHA

MACHI/ APRILI 2015

MUDA: SAA 2 ½

### **MAAGIZO**

1. Andika jina lako na nambari katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.
2. Tia sahihi yako kisha uandike tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.
3. Jibu maswali yote katika nafasi ulizoachiwa katika kijitabu hiki cha majibu.
4. Hakikisha kwamba kurasa zote zimepigwa chapa.
5. Majibu yote ni lazima yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.

### **KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE**

SEHEMU	UPEO	ALAMA
UFAHAMU		
UFUPISHO		
MATUMIZI YA LUGHA		
ISIMU JAMII		
JUMLA	80	

## 1. UFAHAMU

### **Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali yanayofuatia.**

Vipindi mbalimbali vya historia vimeshuhudia kuibuka kwa magonjwa ya ajabu. Magonjwa hayo yamehangaisha watu na kuzishughulisha bongo za wanasayansi na madaktari katika kutafuta tiba. Magonjwa kama vile tauni, kifua kikuu, homa ya matumbo na ndui ni baadhi ya yale yaliyotisha sana nyakati fulani za historia ya binadamu. Magonjwa haya yaliwaua maelfu ya watu na kutibua mifumo na taratibu za maisha ya watu.

Hata hivyo magonjwa hayo yaliweza kuchunguzwa na kutafutiwa tiba kabla ya kumaliza kabisa kizazi cha binadamu. Lakini hii ni baada ya kuwasukuma maelfu ya watu kaburini. Ulimwengu wa sasa unashuhudia janga jingine la maradhi sugu ya Ukimwi. Neno “UKIMWI” lilitoholewa kutokana na athari za ugonjwa huo mwilini. Neno “UKIMWI” humaanisha Ukosefu wa Kinga Mwilini, ambapo herufi za kwanza za maneno matatu ziliunganishwa pamoja na kuunda neno hilo. Ugonjwa huu ambao tayari umewaua mamilioni ya watu kote ulimwenguni unazidi kuenea kwa kasi, mfano wa moto katika kichaka. Kutokana na kasi yake ya kuua watu, ugonjwa wa UKIMWI umepewa majina kama vile ‘umeme’ na pia ‘ugonjwa wa vijana’. Watu wengi wanaoambukizwa virusi vya UKIMWI ni wale walio na miaka kati ya 15 hadi 49. Kundi hili kwa kweli ndilo, linalohesabiwa kuwa na nguvu za kutunza jamii kwa njia nyingi. Iwapo wengi katika kundi hili watakumbwa na maradhi haya, watasalia wakongwe na watoto wasioweza kujimudu.

Nchini Kenya, UKIMWI uligunduliwa kwa mara ya kwanza mnamo mwaka wa 1984. Kufika mwezi wa Juni 1996, inakisiwa kuwa ugonjwa huu ulikuwa umewaua watu wapatao 65,647 nchini . Hivi sasa, inasemekana kuwa takriban watu zaidi ya 500 hufa kila siku nchini Kenya kutokana na janga hili. Aidha, imethhibitishwa kwamba takriban wafu milioni mbili u nusu tayari watapoteza maisha yao kutokana na kuambukizwa virusi vya ugonjwa huu humu nchini. Maradhi haya sasa yamekuwa janga la kitaifa.

Kutokana na kuongezeka kwa visa vya UKIMWI, hospitali na zahanati nyingi kote nchini zinashindwa kukidhi mahitaji ya wagonjwa. Kwa hivyo makundi ya kujitolea na mashirika mbalimbali yameundwa ili kuwashudumia wagonjwa wa UKIMWI. Baadhi ya makundi hayo hutoa tiba ya

kisaikolojia pamoja na kuwapa ushauri wa hima ya kuishi, badala ya kukata tamaa. Wagonjwa wengi pia huishia kutibiwa nyumbani kwao.

Lakini jambo la kuzingatia ni hili, tujifunze kutokana na historia. Tuwe na matumaini kwamba siku moja tiba ya ugonjwa huu itapatikana. Hii ni kwa sababu tumethibitishiwa haya kutoka katika historia yetu wenye. Ikiwa magonjwa yaliyosababisha vifo vya wengi kutokana na ukosefu wa tiba yalitokomezwa kuititia juhudzi za kimatibabu, sembuse huu ugonjwa tulio nao sasa? Huku tukijikinga kutokana na maradhi haya tusife moyo bali tuwe na matumaini kwani subira huvuta heri.

### **Maswali**

- a) Fafanua maana ya vifungu vifuatavyo i)  
Kutibua mifumo na taratibu za maisha ya watu. (Alama 1)

.....  
.....  
.....

- ii) Kuwasukuma maelfu ya watu kaburini. (Alama 1)

.....  
.....

- b) Eleza aina ya magonjwa yafuatayo:-

- i) Homa ya matumbo (Alama 1)

.....  
.....

- ii) Kifua Kikuu (Alama 1)

c) Kwa nini ugonjwa wa UKIMWI umepewa majina ya kimajazi? (Alama1)

---

---

d) Eleza madhara yoyote matatu ya UKIMWI kulingana na taarifa  
(Alama3)

---

---

e) Ni harakati zippi zinazoendelezwa kukumbana na janga hili? (Alama2)

---

---

f) Eleza mienendo inayopaswa kuendelezwa kuondoa kukata tamaa (Alama3)

---

---

g) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumiwa katika taarifa.

i) Takriban..... (Alama 1)

ii) Hima ya kuishi..... (Alama 1)

## MUHTASARI

Imesemwa na kurudiwa tena kwamba, iwapo tuna maono ya kujiondoa katika umasikini wa kupindukia, ni lazima tukipe kilimo umuhimu. Zaidi ya Wakenya milioni 10 wamo hatarini ya kufa njaa katika maeneo mbali mbali kwa sasa kufuatia uhaba wa chakula nchini.

Kiini kikubwa cha njaa hiyo ni mapuuza ya muda mrefu katika sekta ya kilimo. Imesahaulika kuwa karibu asilimia 75 ya Wakenya wanategemea kilimo kwa chakula na mapato ya kifedha kila siku. Kilimo hutoa karibu robo tatu ya nafasi za kazi kwa wananchi na pia kuiletea serikali karibu robo ya mapato yake kutokana na mazao ya mauzo katika mataifa ya nje.

Wataalamu wa masuala ya zaraa wanaeleza kuwa pato la nchi linalotokana na kilimo huangamiza njaa mara nne zaidi ya mapato yanayotokana na shughuli nyinginezo za kiuchumi. Hiyo ni kwa sababu shughuli za kilimo hulenga kuzalisha vyakula moja kwa moja. Imebainika kuwa, katika mataifa mengi yanayostawi, asilimia 75 ya wananchi huishi katika maeneo ya mashambani na idadi hii hutegemea kilimo kujimudu kimaisha ilhali hapa Kenya ni asilimia nne pekee ya bajeti inayowekezwa katika kilimo.

Kwa wakati huo, ushuru unaotozwa bidhaa za kilimo katika maeneo ya Kusini mwa Sahara umebainika kuwa mkubwa. Hii imepelekea uwekezaji katika kilimo kupungua na hivyo kuchangia kukithiri kwa baa la njaa.

Wakati umewadnia kwa serikali za Afrika na wapangaji wa masuala ya kiuchumi kuweka juhudu maradufu katika kushabikia kilimo ili kumaliza njaa na umasikini.

Kuna haja ya kuwajulisha, kuwahimiza na kuwaelimisha wakulima wa mashamba madogo madogo kwa mfano, kuhusu mihimili ya zaraa kama vile uzalishaji wa matunda na mboga, ufugaji wa ndege, samaki na ng'ombe mbali na kuweka mikakati ya kuanzisha nafasi za kazi katika sekta ya kilimo.

Serikali itafikia lengo hili iwapo itaanza kuhifadhi kilimo, kupunguza gharama za pembejeo za kilimo, kuweka sera zinazodhibiti uuzaaji na ununuzi wa vyakula hasa baina ya mataifa na kuongeza sehemu ya bajeti inayotengewa kilimo.

Bila hiyo hatutakuwa na lingine bali kukimbilia mataifa yaliyostawi kuomba misaada ili kuwanusuru raia wetu kutokana na ghadhabu ya njaa.

## MASWALI

- a) Kwa kutumia maneno kati ya 70-75 eleza ni kwa nini kuna haja ya serikali kutilia maanani na kuimarisha kilimo nchini (alama 6, 1 mtiririko)

## Matayarisho

Jibu

- b) Eleza namna serikali inavyoweza kumaliza njaa na umasikini nchini (maneno 60-70) (alamu 9, 1 mtirirk)

## Matayarisho

Jibu

### **MATUMIZI LA LUGHA**

- a. Eleza kwa kutoa mifano tofauti kati ya ala tuli na ala sogezi. (Alama2)
- 
- 
- 

- b. Tunga sentensi ya neno moja yenyeye mofimu zifuatazo. (Alama 3)

- i. Nafsi ya tatu umoja
  - ii. Wakati uliopita
  - iii. ‘O’ Rejeshi
  - iv. Kitendwa
  - v. Mzizi
  - vi. kiishio
- 

- c. Changanua sentensi ifuatayo kwa kutumia jedwali (Alama 3)

Mkoba ambao uliporwa umepatikana

- d. Onyesha aina mbalimbali za nomino katika sentensi ifuatayo.

Kerubo amerudishiwa Jembe alilonyang'anywa.

(Alama 2)

---

- e. Andika sentensi yakinishi kutokana na ifuatayo

(Alama 1)

Ng'ombe hajakamuliwa maziwa yote

---

- f. Onyesha kishazi huru na kishazi tegemezi katika sentensi hii

Miti iliyokatwa na vibarua jana imebebwa leo asubuhi

(Alama 2)

---

- g. Kwa kutunga sentensi eleza matumizi mawili ya kistari kirefu (Alama 2)
- 

- h. Nyambua kitenzi cha silabi moja kifuatacho katika hali ya kutendea, kutendwa/tendewa na  
kutendeka na kutendeana

(Ku) cha

(Alama 2)

---

- i. Andika sentensi zifuatazo kwa Udogo.

Watu wale ni weusi tititi hawaonekani gizani

(Alama 2)

- j. Andika sentensi ifuatayo katika usemi halisi  
Ruheni alishauriwa na kasisi aache tabia ya ulevi (Alama 2)
- 
- 
- 
- k. Tunga sentensi moja itakayodhihirisha maana ya maneno haya mawili  
Shombo (Alama 2)
- 
- 
- 
- Chombo
- 
- 
- 
- l. Neno ‘tikiti’ hupatikana katika ngeli mbili tofaouti. Taja ngeli hizo na utunge sentensi kwa kila moja. (Alama 4)
- 
- 
- 
- m. Andika sentensi ifuatayo ukitoa kinyume cha maneno yaliyopigwa mstari  
Kijana aliyekwea mlima ule alisifiwa sana (Alama 3)
- 
- 
- 
- n. Kanusha sentensi ifuatayo  
Jamila akiimba vizuri atapewa zawadi (Alama 2)
- 
- 
- 
- o. Onyesha nomino zinazoweza kuundwa kutokana na vitenzi vifuatavyo (Alama 2)

- i. Sarifu .....
- ii. Sebeha .....

p. Eleza maana mbili ya sentensi hii

Shamba letu limelimika (Alama 2)

---

---

---

---

q. Ainisha shamirisho katika sentensi ifuatayo

Mume alimpikia chai mkewe kwa jiko (Alama 3)

---

---

---

---

### **ISIMUJAMII**

1. Taja na ufanue nadharia tatu zinazoelezea asili ya lugha ya Kiswahili

(Alama 6)

---

---

---

---

---

---

2. Eleza maana ya istilahi zifuatazo za isimujamii

(a) Lafudhi (Alama 2)

(b) Rejesta

(Alama 2)

---

---

JINA.....NAMBAKI.....

SHULE.....SAHIHI.....

TAREHE.....

102/3

KISWAHILI

KARATASI YA 3

FASIHI

MACHI/ APRILI 2015

MUDA: SAA 2 ½

### **TATHMINI YA PAMOJA YA LAINAKU**

*Cheti cha Kuhitimu Elimu ya Sekondari (K.C.S.E)*

102/3

KISWAHILI

KARATASI YA 3

FASIHI

MACHI/ APRILI 2015

MUDA: SAA 2 ½

MAAGIZO

1. Jibu maswali manne pekee.
2. Swali la kwanza ni la lazima.
3. Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki, yaani Riwaya, Tamthilia, Ushairi na Fasihi Simulizi.
4. Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja.
5. Majibu yote lazima yaandikwe kwa kugha ya Kiswahili.

### **KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE**

SWALI	1	2	3	4	5	6	7	8	JUMLA
TUZO									

### **SEHEMU A: HADITHI FUPI**

#### **(Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine – Ken Walibora)**

##### **1. LAZIMA**

Ilikuwa wakati fulani nikaamua kupata jiko. Niliangaza macho kijiji ni kwetu na janibu za karibu.

- a. Eleza muktadha wa dondoo hii (alama 4)
- b. Tambua na ufanue jinsi mwandishi alivyotumia fani yoyote moja kusanifu dondoo hili ( alama 2)
- c. Onyesha nafasi ya mneni kwenye hadithi (alama 4)
- d. Mtunzi anaangazia maswala nyeti katika hadithi hii. Taja na ueleze yoyote matatu (alama 6)
- e. Taja na ueleze sifa zozote mbili za mnenaji (alama 4)

### **SEHEMU B: RIWAYA**

#### **KIDAGAA KIMEMWOZEA – KEN WALIBORA**

Jibu swali 2 au 3

2. “Wapuuzi hawa. Na haya ya kudai sikuandika riwaya yenyewe ni nani kawaambia. Nilidhani ni siri hii?”
  - a. Eleza muktadha wa dondoo hili (alama 4)
  - b. Taja wahusika wengine wawili walio na siri kisha ueleze kwa ufupi siri zao (alama 4)
  - c. Fafanua sifa za mnenaji (alama 12)
3. ‘Baada ya dhiki faraja’. Fafanua ukweli wa kauli hii kwa kurejelea mifano mwafaka kutoka riwaya ya Kidagaa Kimemwozea.(alama 20)

### **SEHEMU C: TAMTHILIA**

#### **MSTAHIKI MEYA – TIMOTHY AREGE**

Jibu swali 4 au 5

**4. "Hata hivyo inavunja moyo kuona mambo kama haya..."**

- a) Weka maneno haya katika muktadha wake. (Alama 4)
- b) Ni mambo gani haya anayoyarejelea mnenaji? (Alama 4)
- c) Kwa maoni yako, mambo haya yanayorejelewa yanaweza kurekebishwaje? (Alama 4)
- d) Eleza sifa za mnenaji katika dondoo. (Alama 6)
- e) Taja na ueleze fani ya lugha iliyotumika katika dondoo hili. (Alama 2)

5. Hali ya maisha ya watu wa Cheneo ni mfano wa msumari wa moto juu ya kidonda. Eleza.

(Alama 20)

**SEHEMU D: USHAIRI**

Jibu swali 6 au 7

**6. Soma shairi hili kisha ujibu maswali yanayofuata.**

Wote:  
Tualifungua dimba, kwa fujo na hamaki  
Twataka kweli kuamba, yalipo kweli na haki  
Mashaka yalotukumba, vijana na mashabiki  
Madawa haya ya kulevya, ni kitanzu twajitia.

Wasichana:  
Tumejitia kitanzu, kwa kuvuta ino bangi  
Tumepanda hilo penzi, kwa kupumbazwa na bangi  
Tumekuwa kama panzi, 'liyezamaa kwa mtung  
Madawa haya ya kulevya, ni kitanzu twajitia.

Wavulana:  
Si sigara si pombe, kwa vyovyote twajifunga  
Si hiroini si gulu, hivyo vyote twavipanga  
Si chang'aa si dope, vyote hivyo twavitwanga

Madawa haya ya kulevya, ni kitanzitwajitia.

Wasichana : Baada ya pafu moja, ulimwengu huwa tamu  
Timuka moja kwa moja, kutafuta tamu tamu  
Walakini tamu tamu, hugeuka kuwa sumu  
Madawa haya ya kulevya, ni kitanzitwajitia.

Wavulana: Ukimwi hata kaswende, utapata ndugu yangu  
Tatembea kama mende, aliyepigwa kwa rungu  
Utatokwa na umande, kwa kupatwa na uchungu  
Madawa haya ya kulevya, ni kitanzitwajitia.

Wasichana: Tumewaona hao wengi, wamejitunga sindano  
Wakaongeza na bangi, wapate singizi pono  
Wamegeuka mitungi, siyopandwa kono kono  
Madawa haya ya kulevya, ni kitanzitwajitia

Wavulana: Aliyekwambia nani, bangi hutuliza bongo?  
Eti 'kiwa matatani, vuta vuta kimpaongo!  
Wajitia uyawani,kuharibu wako ubongo  
Madawa haya ya kulevya, ni kitanzitwajitia.

Wasichana: Darasani ni kulala, kwa sababu ya madawa  
Watamani kula kula, kwa sababu ya madawa '  
Tabaki kisomo bila, ushindwe hata tibiwa  
Madawa haya ya kulevya, ni kitanzitwajitia.

Wavulana: Usije kashawishika, na hao wako marafiki  
Wakwambie shika shika, ndiposa uwe shabiki  
Madawa haya kuyashika, ni nyumba kweli kubaki  
Madawa haya ya kulevya, ni kitanzitwajitia.

Wote: Tamatini tumefika, ni onyo twalitoeni  
Mzigo utajitwika, madawa kuyaleweni  
'Tajikuta umeshika, tama yako 'kilieni  
Madawa haya ya kulevya, ni kitanzitwajitia.

### **Maswali**

- i. Eleza ujumbe unaojitokeza katika kibwagizo cha shairi hili. (Al.2)
- ii. Katika ubeti wa tatu malenga ametumia mizani "si". Eleza mbinu hii huitwaje na uonyesha kwa nini imetumika katika shairi. (Al. 4)
- iii. Ni madhara gani ambayo yanetajwa yanayoletwa na madawa ya kulevya. (Al. 4)
- iv. "Wamegeuka mitungi, 'siyopandwa na kono kono". Malenga anamaanisha nini katika usemi huu. (Al. 3)
- v. Kwa nini shairi hili linaweza kuitwa ukaraguni. {Al. 2}
- vi. Eleza maana ya maneno haya jinsi yametumika kwenye shairi hili.
  - a) Kuamba
  - b) Kitanzitwajitia
  - c) Umande
  - d) Shabiki
  - e) Tama (Al. 5)

## 7. Soma shairi ulilopewa kisha ujibu maswali

Nakuuliza kazungu, ndugu yangu kulikoni?

Umepekiwa majungu, au ni nira shingoni,

Aushi yako mizungu, nena usinifichani,

Mke kupiga mumewe, ni mila au mapenzi?

Tulikuwa tu mbioni, Zainabu kumnasa,

Ukanipiku mwandani, na hata kutoa posa,

Arusi kitamaduni, ya kikwetu na kisasa,

Mke kupiga mumewe, ni mila au mapenzi?

“ Mabaki kulia ngoa, wingu jeusi “Metanda,

Mahari ulishatoa, vibuzi kuku na punda,

tosi akudonoa, mfano kanga wa manda,

Mke kupiga mumewe, ni mila au mapenzi?

Wikendi ikitimia, Kazungu u mashakani,

Deki wairaukia, maana kuna wageni,

Kahawa wajipikia, Mkeo yu kitandani,

Mke kupiga mumewe, ni mila au mapenzi?

Mshahara “ Kipokea, Mkabidhi mkononi,

Kidogo akugawia, uendee kinyozini,

Nje ukichelewa, Utalala ukumbini,

Mke kupiga mumewe, ni mila au mapenzi?

Wewe u Kamili mume, au kafiri njusi,  
Songa mbele umseme, tuone akikutusi,  
Amuri yake mtume, Hapo umpe divosi,  
Mke kupiga mumewe, ni mila au mapenzi?

***Maswali***

- a) Lipe kichwa shairi ulilosoma (Alama 2)
- b) Kwa kutoa sababu kamili, litie shairi hili katika bahari zozote nne. (Alama 4)
- c) Je shairi hili lina kibwagizo? Eleza (Alama 2)
- d) Eleza muundo wa ubeti wa pili. (Alama 4)
- e) Kwa kutoa mifano mwafaka, Onyesha jinsi msanii ametumia uhuru wake.  
(Alama 4)
- f) Eleza msamiati ufuatao jinsi ulivyotumika katika shairi.
  - i) Ukanipiku
  - ii) Nira
  - iii) Aushi
  - iv) Posa (Alama 4)

**SEHEMU E: FASIHI SIMULIZI**

8. (a) Tunakusifu ewe mfalme wetu,  
Hakuna wa kulinganishwa nawe,  
Ushujaa wakoni ule wa simba,  
Tutaendelea kukariri wema wako.

- i) Maelezo haya yanapatikana katika utanze na kipera gani cha Fasihi Simulizi?(  
Alama 2)
- ii) Tambua sifa za kipera hiki. (Alama 4)
- iii) Eleza umuhimu wa kipera hiki katika jamii.  
(Alama 4)

b) Tofautisha:

- i) Maghani na mighani ( Alama 2)
- ii) Ulumbi na soga (Alama 2)
- iii )Mawaidha na mazungumzo (Alama 2)
- iv) Misimu na misemo (Alama 2)
- v) Lakabu na malumbano ya utani (Alama 2)